

Majukumu ya Idara ya Ardhi na Maliasili

- Kuratibu uandaaji wa Mipango ya kimbinu ya kuendeleza Miji (Strategic Urban Development Plan).
- Kuratibu uandaaji wa mipango ya maeneo yaliyoendelezwa kiholela.
- Kuandaa michoro ya mipangomiji.
- Kutoa masharti ya uendelezaji wa Ardhi.
- Kupokea michoro ya Mipangomiji na taarifa za maeneo ya ardhi yanayopendekezwa kuiva kwa ajili ya uendelezaji kimji.
- Kuchambua takwimu na taarifa kwa ajili ya maandalizi ya mipango mipya ya makazi.
- Kupokea na kuweka kumbukumbu za maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi na umegaji wa viwanda.
- Kuhakikisha kwa mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanaingizwa katika michoro.
- Kusimamia/Kuthibiti uendelezaji wa makazi.
- Kuratibu uandaaji wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji.
- Kutoa ushauri wa uendelezaji wa ardhi kwa wananchi.
- Kukagua kazi za Upimaji.
- Kupima maeneo mbalimbali (Mashamba na viwanja).
- Kuandaa michoro kwa ajili ya Hatimiliki za kisheria.
- Kutunza kumbukumbu za Upimaji.
- Kurudisha mipaka.
- Kuhifadhi na Kutunza Misitu na Mazingira.
- Kuhimiza na kusimamia upandaji wa miti na kutunza misitu vijijini.
- Usimamizi, ulinzi na utunzaji wa misitu na rasilimali zake.
- Usimamizi wa sheria za Misitu.
- Kusimamia, na kufuatilia makusanyo na ushuru wa mazao ya misitu.
- Ulinzi na usimamizi wa vyanzo na kinga za maji, utunzaji wa udongo na ulinzi wa mimea.
- Kusimamia hifadhi za misitu na kutoa elimu kwa jamii.
- Kusimamia shughuli zote za ufugaji nyuki vijijini.
- Kutunza mazingira ya nyuki yaliyopo pamoja na kupanda miti ifaayo kwa nyuki.
- Kuhamasisha na kueneza kwa jamii na wanavijiji kufuga na kutunza nyukii kisasa.
- Kuhamasisha jamii kutengeneza mizinga ya kisasa ya gharama nafuu kwa kuzingatia mazingira yao
- Kuunda na kusimamia vikundi vya ufugaji nyuki vijijini.
- Kusimamia mazao ya ufugaji nyuki.
- Kutoa elimu kwa jamii kuhusu ufugaji nyuki wa kisasa huko vijijini.
- Kuhamasisha watu binafsi taasisi mbalimbali kufuga nyuki kwa lengo la kujiongezea kipato na lishe.
- Kutunza mazingira na wanyamapori.
- Kusimamia shughuli zote za wanyamapori vijijini.
- Kulinda watu na mazao kutohariibiwa na wanyamapori.
- Kushughulikia leseni za uwindaji wa wanyamapori.

- Kulinda wanyamapori.

UTEKELEZAJI IDARA YA ARDHI

Idara ya ardhi imeweza kutekeleza yafuatayo;

MALENGO	UTEKELEZAJI
Kupima viwanja	Hadi kufikia 2015, jumla ya viwanja 5,541 vimepimwa katika eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo Mlandizi. Zoezi la upimaji linaendelea.
Kutoa Hati Miliki za Ardhi	Hadi kufikia 2015, jumla ya Hati Miliki 3,050 zimetolewa kwa viwanja vilivyopimwa mamlaka ya Mji Mdogo Mlandizi. Zoezi linaendelea.
Kupima Mipaka ya Vijiji	Hadi kufikia 2015, jumla ya Vijiji 21 vimepimwa. Zoezi linaendelea.
Kujenga Masjala za Ardhi Wilayani na Vijijini	Hadi kufikia 2015, jumla ya Vijiji 9 ambavyo ni Mpiji Station, Kipangege, Soga, Kwala, Misufini, Dutumi, Minazi mikinda, na Lukenge vimejenga Ofisi Imara ambazo zinaweza kutumika kuifadhi nyaraka za Kumiliki Ardhi. Zoezi linaendelea katika maeneo mengine yaliyobaki.